Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

# MATUKIO YA SUA

*Julai - Septemba, 2024*



**Ardhi ni Hazina**

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 1 | Bodi ya Uhariri. |
| 2 | Wahitimu SUA katumieni elimu bora mliyopata chuoni kutatua changamoto za wakulima - Mhe. Rais Samia |
| 5 | SUA kuanzisha Msitu wa Chuo wa Mafunzo ya Biashara mkoani Ruvuma |
| 6 | SUA yajivunia ushirikiano na Chuo Kikuu cha Kilimo cha China |
| 7 | Rais Samia aipongeza SUA |
| 9 | "Taasisi za utafiti na za mafunzo ya misitu endeleeni kubuni mbinu na teknolojia rahisi kwa ajili ya wenye ujuzi na mitaji midogo" Waziri Kipanga |
| 11 | Wakulima watakiwa kupima udongo kwa Uzalishaji wenye tija katika kilimo |
| 12 | Zao la Kahawa kulimwa popote kama mkulima akizingatia mbegu bora, huduma na Elimu |
| 13 | Watafiti SUA wabaini Bioanuai 3935 kwenye Safu za Milima ya Tao la Mashariki |
| 14 | Vijana 300 kutoka SUA kukwamuliwa kiuchumi kila mwaka |
| 15 | Wanafunzi wa SUA wakubalika zaidi katika Soko la Ajira |
| 16 | Wanafunzi wa Wilbalda Sekondari wafanya Ziara SUA kujifunza kilimo kwa vitendo |
| 17 | Kampuni ya Uzalishaji wa Sukari Bagamoyo yaipongeza SUA kwa kutoa wahitimu bora |
| 18 | SUA kushirikiana na Halmashauri ya Mpimbwe kutoa elimu na tafiti kwa wakulima na wafugaji |
| 19 | Watumishi epukeni mgongano wa maslahi |
| 20 | RC Malima awataka wataalamu wa misitu sua kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu |
| 22 | SUA yanunua Mtambo wa kuchimba visima |








## *Bodi ya uhariri*

### Wataalamu wa Mawasiliano na Masoko

**Bi. Suzana Magobeko**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko

Bw. Asifiwe Mbembela
Afisa Mawasiliano na Masoko

### Mhariri Mkuu

**Dkt. James Nyangas**
Mkuu wa Idara ya Elimu ya Saikolojia na Unasihi.

### Mhariri

**Bw. Absolome Senzige**
Mhadhiri Msaidizi

### Wasanifu

**Bw. Rajab Kimaro**
**Bi. Jackline Japhet**







***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiongea na mamia ya watu waliojitokeza katika hafla ya uzinduzi wa Jengo la Mafunzo la Dkt. Samia Suluhu Hassan uliofanyika tarehe 6 Agosti, 2024 katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro.***

# Wahitimu SUA katumieni elimu bora mliyoipata chuoni kutatua changamoto za wakulima - Mhe. Rais Samia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kuitumia elimu bora ya kilimo wanayoipata chuoni hapo kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili wakulima nchini.

Rais Samia alitoa kauli hiyo Agosti 6, 2024 wakati akizungumza na wanajumuiya ya SUA baada ya kuzindua Jengo Mtambuka la Mafunzo liliopo SUA Kampasi ya Edward Moringe na kukipongeza Chuo hicho kwa kutoa elimu yenye ubora wa hali ya juu kwa wanafunzi wake na kusema kuwa anaamini matunda ya wahitimu hao yanaonekana wazi kwa wakulima.

“Matarajio yangu kwa vijana mnaotoka SUA, baada ya sera na mipango yote inayowekwa na SUA katika kutengeneza nguvu kazi ya Tanzania, na namna mnavyotengenezwa hapa, hamtakuja kusumbua sana katika ajira, bila shaka wapo tutakao wachukua kwenye ajira hapa hapa chuoni, kwenye vyuo mbalimbali vya mifugo, vyuo vya kilimo na sekta nyinginezo ambavyo vyote hivyo vinatumika kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu” alisema Mhe. Rais Samia.

Alisema kwa ni kiasi kikubwa vijana wanaohitimu SUA watakwenda kuungana kwenye Programu kubwa ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT), na Serikali itajitahidi kutafuta fedha ili kuwapa nguvu wakiwa kwenye Programu hiyo kwa lengo la kukuza ajira lakini pia kukuza Sera ya kilimo biashara.

“Ombi langu kwa wanafunzi wanaohitimu hapa SUA ni kwenda huko kwenye Programu yetu ya BBT, bahati nzuri Waziri Bashe yupo hapa na sasa hivi najua kashavua kofia anakuna kichwa kufikiria namna atakavyoweza kuwaingiza huko na fedha atatoa wapi, lakini Mungu atatufungulia njia tutaweza”, alisema Mhe. Rais Samia.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Mhe. Rais Samia, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda alisema serikali inajivunia sana kazi nzuri za tafiti zinazofanywa na SUA ikiwa ni pamoja na tafiti zilizowezesha kupatikana kwa chanjo ya kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo au kideri na utafiti wa mbegu bora ya maharage inayoitwa Mshindi ambayo inahimili ukame na kustahimili magonjwa.

“Mhe. Rais kuhusu changamoto ya ufadhili ipo, nakumbuka ulituambia wakati tunapotoa vivutio tuwaangalie na Wahadhiri wa vyuo vikuu ambao wanatumia muda mrefu sana kwa ajili ya kufanya uta-

fiti. Kufuatia agizo hilo tayari tumeanza kutoa tuzo ya Shilingi milioni hamsini (50,000,000/=) kwa Mtafiti yeyote ambaye utafiti wake utakubalika kimataifa na kigezo cha kimataifa ni kuchapisha majarida ya hali ya juu zaidi duniani, lakini niseme tu ili kuweza kutekeleza agenda ya kuibua tafiti hatuna budi kutafuta fedha kwa ajili ya kuwawezesha watafiti nchini", alisema Prof. Mkenda.



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) akiongea wakati wa hafla ya uzinduzi wa Jengo la Mafunzo la Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro.*



*Picha za matukio mbalimbali wakati wa hafla ya uzinduzi wa Jengo la Mafunzo la Dkt. Samia Suluhu Hassan*



















# SUA kuanzisha Msitu wa Chuo wa Mafunzo ya Biashara mkoani Ruvuma

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimekusudia kuanzisha Msitu wa Chuo wa Mafunzo ya Biashara katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba mkoani Ruvuma ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya Chuo hicho ya kusimamia na kuongeza uzalishaji wa mapato ya ndani ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mhe. Jaji Mohamed Chande Othman wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa Jengo Mafunzo la Dkt. Samia Suluhu Hassan Agosti 6, 2024 katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro ambapo Mgeni Rasmi alikuwa ni Rais wa Jamuhri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

"Msitu huo utakuwa na ukubwa wa hekta 10,000na tutautumia kwa ajili ya biashara ya Kaboni na uzalishaji wa mazao mengine ya misitu, hii inakwenda sambamba na kununua vifaa vya kisasa vya kuchaka magogo", amesema Mhe. Jaji Othman.

Mhe. Jaji Othman ameitaja mikakati mingine kuwa ni: kuanzisha Kampuni ya uwekezaji wa Chuo na kwamba kampuni hiyo itasimamia vitengo vyote vya uzalishjai ambavyo sio vya kitaaluma vyenye uwezo wa kuzalisha mapato chuoni, kuimarisha Shamba la Biashara la Chuo lililopo Kampasi ya Solomon Mahlangu pamoja na vitengo vyote kikiwemo Kitengo cha Maziwa, Nguruwe, Shamba la Uzalishaji wa Chakula cha Mifugo na kuendelea kupanda Mkonge ambapo mpaka sasa hekari 200 zilishapandwa na mwaka huu zitavunwa hekari 100.

"Pia Baraza la Chuo linaendelea kutunga na kuboresha sera, kanuni na miongozo ya ndani kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Chuo katika maeneo yote ya kimkakati kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na Serikali ili kuhakikisha Chuo kinatekeleza majukumu yake ipasavyo", amesema Mwenyekiti huyo wa Baraza la Chuo SUA.



***Mhe. Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.***



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea zawadi ya mche wa matunda aina ya mwembe kutoka kwa Mkuu wa Chuo Mhe. Jaji Joseph Warioba.***

# SUA yajivunia ushirikiano na Chuo Kikuu cha Kilimo cha China

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kinaendelea kujivunia ushirikiano wake na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Shenyang cha nchini China ulioanza mwaka 2017.

Akizungumza na SUA Media Agosti 12, 2024 baada ya kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Chuo cha Kilimo cha Shenyang pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha SUA Prof. Raphael Chibunda, Prof. Japhet Kashaigili ambaye ni Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, na Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam alisema kuwa wamekutana kwa lengo la kuyapitia makubaliano waliyoingia mwaka 2017 na kuangalia namna ya kuyaendeleza.

Alisema kuwa moja kati ya makubaliano hayo ilikuwa ni kubadilishana wataalamu pamoja na wanafunzi, na kuwa Chuo Kikuu cha SUA kimeshanufaika na mashirikiano hayo na kuwa kuna idadi ya wataalamu ambao wameshakwenda kusoma katika Chuo hicho na sasa wanaendelea kufanya shughuli zao hapa chuoni.

Pia, Prof. Kashaigili alisema katika kikao hicho wamejadili namna ya kuyaendeleza makubaliano hayo na kufanya zaidi ya hapo kwa kuanzisha programu maalumu ya kibiashara ya kimataifa ya kilimo na kupeleka walimu wengi zaidi kutoka SUA kwenda China na wataalamu wa Chuo hicho kuja SUA.

Aidha Prof. Kashaigili alibainisha kuwa muendeleo wa makubaliano hayo na urafiki kati ya vyuo hivyo viwili utaleta manufaa kwa Chuo Kikuu cha SUA pamoja na taifa kwa ujumla kwa maana utalaamu huo ukija hautaishia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

“Maendeleo haya ni endelevu na yana faida kwa Chuo chetu na kwa Nchi kwa ujumla kwa maana utaalamu ukija hauishii tu kwa Chuo chetu bali utasambaa kwa taifa zima”, alisema Prof. Kashaigili.

Naye Makamu wa Rais wa Chuo hicho cha Kilimo cha Shenyag, Prof. Li Bin alisema kuwa lengo lililowaleta SUA ni kupitia makubaliano waliyoingia awali na pia kuanzisha makubaliano mapya.




*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu SUA Prof. Raphael Chibunda (kushoto) akijadili jambo na Makamu wa Rais wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Shenyang cha nchini China Prof. Li Bin.*





# Rais Samia aipongeza SUA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akionesha kitabu cha "Edward Moringe Sokoine: Maisha na Uongozi Wake" mara baada ya kukizindua katika hafla iliyofanyika kwenye Ukumbi wa JNICC Jijini Dar es Salaam 30 Septemba, 2024.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kufanikisha mchakato wa uandishi wa kitabu cha aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Hayati Edward Moringe Sokoine.

Rais Samia alitoa pongezi hizo wakati akizindua wa kitabu cha Uongozi na Maisha ya Hayati Sokoine Jijini Dar Es salaam katika ukumbi wa JNICC.

Alisema kuwa SUA kimekuwa Chuo kinachoishi maono ya Hayati Sokoine mpaka sasa na kufanya historia yake iendelee kuishi kwa kupitia Chuo hicho

Aidha, Mhe. Rais aliwataka vijana hususani viongozi vijana kuwa wachapakazi kama alivyokuwa Hayati Sokoine na hata kuaminiwa akiwa na umri mdogo na kupewa madaraka makubwa ya kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania. Pia amewaomba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwawezesha viongozi walio hai waweze kuandika historia zao kwenye vitabu .

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba alimuelezea Hayati Sokoine kama kiongozi shujaa na aliyeweza kuishi maisha ya kimaskini, lakini pia akisimamia sheria kwa ajili ya kupambana na wabadhilifu na wala rushwa nchini, huku akitoa mifano mbalimbali ya wakati wa uhai wake.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo cha SUA Prof. Raphael Chibunda alielezea chimbuko la Chuo cha Sokoine cha Kilimo huku akiweka wazi uhusiano uliopo kati ya Waziri Mkuu huyo na Chuo hicho huku akieleza namna maamuzi ya kuanzishwa kwa Chuo hicho yalivyotolewa na Waziri Mkuu huyo Aprili 11 mwaka 1984 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Prof. Chibunda aliongeza kuwa Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimekuwa kikimuenzi Hayati Sokoine kila mwaka kuanzia mwaka 1992 kwa kufanya mihadhara wa kumuenzi.

*Baadhi ya picha zikiwaonesha viongozi wa Serikali akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, viongozi wa SUA na Watumishi kutoka Mashirika na Taasisi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa kitabu cha "Edward Moringe Sokoine: Maisha na Uongozi Wake"*















*Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaye pia ni Mbunge wa Mafia Mhe. Omary Kipanga (katikati) akiwa na viongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na viongozi wengine wa Serikali.*

# Taasisi za utafiti na mafunzo ya Misitu zimetakiwa kubuni mbinu na teknolojia rahisi

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hapa nchini imezitaka taasisi za utafiti na zile zinazotoa mafunzo ya misitu kuendelea kubuni mbinu na teknolojia rahisi kwa ajili ya wananchi wa vijijini wenye ujuzi na mitaji midogo ili kuwawezesha kutumia ipasavyo rasilimali za misitu kwa njia endelevu na yenye manufaa kwa taifa na vizazi vijavyo.

Agizo hilo lilitolewa na Naibu waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga (Mb) kwenye maadhimisho ya jubilei ya miaka 50 ya utoaji wa taaluma za misitu katika Chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo yaliyofanyika katika Chuo hicho. Mhe. Kapinga alisema kuwa SUA inapaswa kuona umuhimu wa kuwa na mikakati thabiti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, Mhe. Kipanga alisema kuwa nafasi ya sekta ya misitu katika maisha ya binadamu na katika maendeleo ya taifa la Tanzania ni kubwa kama ambavyo utafiti unavyoeleza kuwa eneo la misitu kwa Tanzania ni takribani hekta milioni arobaini na nane ambalo ni sawa na asilimia hamsini na tano ya ardhi yote ya Tanzania bara

Hata hivyo alisema kuwa umuhimu wa sekta ya misitu huonekana pia katika maeneo yaliyoainishwa mpango wa maendeleo ya taifa na maendeleo endelevu ya umoja wa mataifa. Wataalamu wa misitu 2630 wamehitimu mafunzo hayo kwa ngazi mbalimbali ambao wanasimamia rasilimali za misitu ndani na nje ya taifa la Tanzania.

“Kwa hapa nchini wataalamu hawa wamewezesha kutengwa kwa hekta milioni arobaini na nane nukta moja (48,100,000 ha) ya hifadhi za misitu pamoja na uanzishwaji wa hekta laki tano themanini na mbili elfu na mia saba ishirini na tisa (582,729 ha) za mashamba ya misitu ya kibiashara” Kipanga alisema.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo, Prof. Raphael Chibunda alieleza kuwa Menejimenti ya Chuo hicho pamoja na wafanyakazi wa kitivo cha misitu wanakitazama kitivo hicho kwa jicho la kipekee na wanamikakati ya kukifanya kuwa kitivo cha umahiri kutokana na SUA kuwa Chuo kiongozi kwenye sekta ya misitu katika ukanda wa SADC na nchi za Afrika Mashariki.

“Kupitia maadhimisho hayo, menejimenti na wafanyakazi tuna kila sababu ya kujitathmini juu ya sekta ya misitu na namna ya kudhibiti uharibifu wa misitu na namna bora ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi” Prof. Chibunda alisema.


Mkuu wa wilaya ya Morogoro, Mhe. Mussa Kilakala alisema, kuwa upekee wa taaluma ya misitu inayotokana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo taifa la Tanzania pamoja na mataifa mengine yameshuhudia matokeo makubwa katika sekta ya misitu yaliyotokana na uwepo wa kitivo cha misitu katika Chuo hicho.

Hata hivyo, amewataka vijana na wataalamu waliosoma katika Chuo hicho na watanzania kwa ujumla kuenzi jitihada za waasisi wa Chuo hicho akiwemo Hayati Edward Moringe Sokoine, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na waasisi wengine.

*Baadhi ya picha za matukio wakati wa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Mafunzo ya Taaluma ya Misitu Nchini tangu kuanzishwa kwake 1973*














*Mkuu wa Maabara kutoka Idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Bw. Amour Mohamed*

# Wakulima watakiwa kupima udongo kwa Uzalishaji wenye tija katika kilimo

Wakulima wametakiwa kuzingatia upimaji wa udongo katika mashamba yao kabla ya kuanza kupanda mazao ili kutambua ubora wa udongo, kilimo anachotakiwa kulima pamoja mbolea ya kutumia ili kufanya uzalishaji wenye tija kwa maslahi binafsi na Taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Maabara kutoka Idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Bw. Amour Mohamed alibainisha kuwa upimaji wa udongo, unasaidia kutambua ubora na afya ya udongo ambapo maabara hiyo ya udongo inampa uwezo mkulima kwa kumpa majibu ya maeneo sahihi ya kulima kulingana na mazao husika.

Aidha alisema kuwa kupima udongo kuna faida ya kumfanya mkulima kutambua Tindikali, Naitrojeni, Fosforasi, Potashiam, Chumvi (EC) pamoja na aina ya udongo vitu ambavyo vinamsaidia kufanya uchaguzi wa mbolea atakazotumia shambani na mazao gani anaweza kulima katika eneo hilo.

Mkuu huyo Maabara alisema wakulima wengi wamekosa elimu ya upimaji udongo kabla ya kuanza kilimo na kujihusisha na kilimo cha mazoea ambacho hakina faida kwao, hivyo ni wakati muhimu sasa kwa wao kutambua elimu hiyo ya afya ya udongo na mimea pasi kusubiri kupeleka sampuli zao za udongo katika maabara baada ya kuona madhara kwenye mimea.

Aliongeza kuwa, mbali na kupima afya ya udongo, katika Idara iyo pia wanapima mazao na samaki ili kutambua ubora wake kwa mlaji pamoja na kuangalia kiwango cha madini tembo (Heavy Metal) ambayo yanapatikana kwenye udongo au madawa yatumikayo shambani kwani yakizidi hupelekea magonjwa mbalimbali kwa mlaji ikiwemo kansa.

Katika hatua nyingine, Bw. Mohamed alisema SUA imekuwa na kawaida ya kuwatembelea wakulima sehemu walipo pindi panapokuwa na mradi ambao unalipa gharama zote lakini kwa sasa wakulima wanatakiwa kufika wenyewe kwenye maabara hiyo ili kufanya vipimo na kupata ushauri wa kubadili mazao ili kuepuka hasara zinazopatikana kwa kufanya kilimo cha mazoea.





# Zao la Kahawa kulimwa popote kama mkulima akizingatia mbegu bora, huduma na elimu

Wananchi hasa wakulima nchini wametakiwa kujua elimu ya ulimaji wa zao la kahawa, jinsi ya kulihudumia zao hilo na namna ya upatikanaji wa mbegu bora ambapo kwa kuzingatia hayo upo uwezekano wa kulima zao hilo kwenye eneo lolote.

Hayo yalibainishwa na Bw. Godwin Rwezaula ambaye Afisa Kilimo Mwandamizi kutoka Ndaki ya Kilimo, Idara ya Mimea Vipando na Mazao ya Bustani katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, wakati akizungumza na SUA Media kuhusiana na elimu ya zao la kahawa kwa wakulima na uzalishaji wake kitaalamu ili kujiongezea kipato chao na cha Taifa kwa ujumla.

Alisema kuna aina kuu mbili za kahawa zinazozalishwa SUA ambazo ni Robusta na Arabika. Kati ya hizo kuna aina nyingine nyingi ambazo zimetoka katika Taasisi ya Utafiti Arusha na wao wanazifanyia utafiti ili kuzijaribu na kuona kiikolojia kama zinaweza kulimwa vizuri Mkoani Morogoro

Aidha, Bw. Rwezaula alisema kwa kawaida kahawa hulimwa na kustawi vizuri sehemu za ukanda wa juu kama Kilimanjaro, Kigoma, Tabora, Mbeya pamoja na Mbinga na kwa Mkoa wa Morogoro zao hilo linaweza kulimwa vizuri katika maeneo ya ukanda wa juu kama vile Kinole, Matombo na Mkuyuni, Hivyo wao kama SUA, kupitia tafiti wanazofanya wamegundua kuwa hata ukanda wa chini zao hilo linaweza kustawi vizuri endapo mkulima atazingatia namna bora ya ulimaji.

“Zipo aina bora za mbegu ya kahawa ambazo zina uwezo wa kustahimili katika maeneo ya ukanda wa chini hasa kwa Mkoa wa Morogoro hivyo mkulima akitambua aina hizo bora za mbegu ya kahawa na kufuata hatua kwa hatua namna bora ya uzalishaji wa zao hilo anaweza akazalisha kwa tija”, amesema Bw. Rwezaula.

Bw. Rwezaula aliongeza kuwa kati ya mambo ya msingi kwa mkulima anayeanza uzalishaji wa zao la kahawa ni lazima kuangalia ikolojia aliyopo kama inafaa kwa ajili ya zao hilo na baadaye kujua chanzo cha vipando ambavyo anahitaji kwa ajili ya kahawa hivyo, kwa sasa wanashauri wakulima wapande kahawa bora kwa njia ya vikonyo ambapo kuna vitalu maalumu vikiwemo vya Serikali.



# Watafiti SUA wabaini Bioanuai 3935 kwenye Safu za Milima ya Tao la Mashariki

Mradi wa Utafiti wa kuongeza matumizi ya taarifa za bioanuai kwa uhifadhi endelevu na kipato kwenye Milima ya Tao la mashariki nchini Tanzania umebaini uwepo wa zaidi ya Bioanuai 3935 kwenye Misitu ya asili ya hifadhi ya Kilombero,Uzungwa na Uluguru.

Akitoa takwimu hizo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu kwa maafisa uhifadhi kutoka kwenye misitu hiyo mitatu ya asili ya hifadhi iliyo kwenye Safu za milima ya Tao la mashariki, Mkuu wa mradi wa utafiti huo Prof. Pantaleo Munishi kutoka Idara ya Mifumo Ikolojia na Uhifadhi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, alisema matokeo hayo ya utafiti yatasaidia wahifadhi kutambua na kuweka mikakati ya namna ya kutunza bioanuai hizo na kuzitangaza ulimwenguni ili kuongeza tija.

"Milima ya Tao la mashariki ni moja ya maeneo muhimu ya Bioanuai yanayotambulika kidunia na kupewa kipaumbele ili kutunzwa na kumekuwapo na miradi mingi ya utunzaji wa misitu na Bioanuai zilizomo lakini kumekuwa hakuna taarifa sahihi za Bioanuai zilizomo katika kipindi chote cha utekelezaji wa miradi hiyo" alifafanua Prof. Munishi.

Akifungua mafunzo hayo ya siku tatu Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Misitu na nyuki wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Ezekiel Mwakalukwa alisema kuwa matokeo mazuri ya utafiti yakitunzwa vizuri kwenye kanzidata moja na kuwezesha upatikanaji wake kirahisi inaweza kusaidia jamii na serikali kufanya maamuzi sahihi ambayo yataleta tija kwa wananchi na taifa.

"Bioanuai ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na taifa na mara nyingi kutokuwa na taarifa zake sahihi katika nchi au misitu kunapelekea uhifadhi wake kuwa mgumu na zingine kutoweka hivyo, tafiti zinasaidia sana kuzitambua lakini kuweka mipango madhubuti ya kuzihifadhi ili ziendelee kutoa mchango stahiki kwenye maendeleo" alieleza Dkt. Mwakalukwa.

Aliongeza, "Nipongeze kazi kubwa iliyofanywa na mradi huu unaaongozwa na Prof. Pantaleo Munishi kutoka hapa SUA kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kufanya utafiti katika misitu yetu mitatu ya hifadhi ya asili iliyo kwenye milima ya Tao la mashariki kubainisha bioanuai muhimu zilimo na kuwezesha taarifa zake kupatikana na hivyo kuwa rahisi kuzitangaza dunaini na kusaidia mipango ya serikali na wasimamizi wa misitu hiyo kupanga mipango bora ya kuzihifadhi".



*Picha ya pamoja na Mgeni rasmi na washiriki wa mafunzo hayo ambao ni maafisa wa uhifadhi kutoka misitu mitatu ya hifadhi ya asili iliyofanyiwa utafiti na Mradi huo.*

# Vijana 300 kutoka SUA kuwezeshwa kujikwamua kiuchumi kila mwaka

Katika kuhakikisha Vijana wanaosoma Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na maeneo jirani wanaweza kujikwamua kiuchumi na kujifunza kwa vitendo kupitia ufugaji wa Kuku, Chuo hicho kinaingia makubaliano ya ushirikiano na Kampuni ya AKM Gritters CO LTD ambapo kwa pamoja wanategemea kuwezesha vijana wapatao 300 kila mwaka.

Akizungumza wakati wa kutoa wasilisho lake, Mkurugenzi wa Kampuni ya AKM Gritters CO LTD Bi. Elizabeth Swai alisema Kampuni yao imeweza kusaidia vijana wengi mkoani Tanga hivyo wameona ni wakati sahihi sasa Tanzania kupitia Chuo Kikuu cha Kilimo cha SUA kuanza kufaidika na fursa hilo kwani kushirikiana kwao kutasaidia kutoa elimu ya masoko, ujasiliamali, teknolojia mpya, menejimenti pamoja na kujitegemea kwa vijana hao kwa kutumia eneo dogo kufuga kuku na kupata faida.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda aliunga mkono ushirikiano huo na kuomba kampuni hiyo kuharakisha nyaraka za mashirikiano hayo ili kuyafanyia kazi na kuhakikisha jambo hilo linafanyika kwa haraka kwani SUA kupitia wao itafaidika sio tu kwa wanafunzi kujifunza lakini pia kuhakikisha wanapata elimu ya kujikwamua kiuchumi kutokana na mafunzo hayo hivyo SUA, itakuwa tayari kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi kutekelezea shughuli hizo.

“Mhe Rais amezitaka Taasisi za Umma zianze kufikiria katika kilimo na imetokana na ung'amuzi mbaya wa Kiwanda cha Sukari kwa hiyo sisi kama tunapata mshirika tukafikiria inayoweza kuwa na pande mbili mafunzo, na wengine wasio na eneo nyumbani wapate mahali pa kujifunzia hapohapo kwenye kituo” amesema Prof. Chibunda.

Kwa upande wake Msimamizi wa Kamati ya Ushauri wa Viwanda kutoka SUA, Dkt. Felix Nandonde alielezea jinsi anavyouelewa mradi huo na kusema kuwa mradi una umuhimu kwa Chuo kutokana na kusaidia vijana na wanawake katika ufugaji kuku, kupata mikopo ya kukuzia biashara zao na kuwafuatilia kwa ukaribu hivyo kushirikiana na SUA ni nafasi kwao kujitanua kwani chuo hicho kinaweza kuchangia maarifa waliyokuwa nayo, ardhi pamoja na vijana wenye hari ya kuzalisha na kuinua tasnia ya kuku.

Akieleza ni kwa namna gani zoezi hilo litakuwa na faida kwa Chuo Mtaalamu wa Kuku kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Bw. Said Mbaga, alisema mradi huo umekuja SUA kwa wakati muafaka kwasababu utasaidia wakati ambapo wanafunzi hawapo kuweza kushughulika na biashara ya kuku tofauti na ilivyo sasa ambapo eneo linalotumika kwa kufugia kuku limekuwa maalum kwa ajili ya kufanyia tafiti peke yake.



*Mkurugenzi wa Kampuni ya AKM Gritters CO LTD Bi. Elizabeth Swai.*



*Makamu Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda.*



# Wanafunzi wa SUA wakubalika zaidi kwenye Soko la Ajira



Matokeo ya Mabadiliko ya Mitaala yanayofanyika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) yamewezesha Chuo hicho kuwa bora zaidi katika kutoa mafunzo yenye tija pia kwa vitendo yanayopelekea kupata ajira kwa haraka inayotokana na kuchagua na kufundisha masomo yanayoweza kumfanya mwanafunzi kujiajiri hata kupata wepesi katika ushindani wa Soko la Ajira.

Zoezi la kufanya Tathmini kupitia Mjadala wa Uzoefu juu ya Mafunzo kwa Vitendo Shahada ya Usimamizi wa Utalii 2024, Idara ya Utalii na Mapumziko Huishi SUA, umeibua mambo muhimu ambayo yamesaidia kuweza kuona mafanikio katika utoaji wa elimu na ufatiliaji wa wanafunzi kwenye mafunzo kwa vitendo kwa lengo la kuendelea kuboresha elimu inayotolewa chuoni hapo.

Akizungumza mara baada ya mjadala huo Profesa Mshiriki kutoka Idara ya Utalii na Mapumziko Huishi SUA, John Mgonja ambaye alikuwa Mwenyekiti wa mjadala huo alisema wanafunzi wa SUA wanaajirika zaidi kulinganisha na vyuo vingine kutokana na heshima ya kazi, kujituma, uwezo wa kutafsiri walichofundishwa na kukiweka katika vitendo nikutokana na kuwa, SUA inatoa fursa ya kufanya mafunzo kwa vitendo kwa miaka mitatu.

Alipozungumzia umuhimu wa kuchagua mafunzo yanayohusiana na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa mwanafunzi, Prof. Mgonja alisema kupitia mabadiliko ya mitaala wameweza kuona vitu muhimu ambavyo vinamjenga mwanafunzi kujiandaa kwenye ajira na kuwasikiliza waajiri nini wanataka hivyo chuo kimechagua masomo muhimu ili wanafunzi wapate kufahamu kulingana na mahitaji ya soko ikiwemo sehemu ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwani ni kozi nzuri inayomjenga mwanafunzi kuwa salama katika sehemu ya kazi.

Kwa upande wake Mhadhiri kutoka Idara ya Utalii na Mafunzo Uhishi SUA, Ernest Mwamwaja alisema kupitia mafunzo kwa vitendo wanafunzi kutoka SUA wamejitofautisha na wengine kutokana na ubora wao wa kuonesha ubunifu ambao amewahahakikishia wazazi, walezi kuwa mwanafunzi anaposoma Kozi ya Utalii na Mapumziko Huishi kwa miaka mitatu atakuwa na uwezo wa kufanya kazi zake kwa ufanisi wa hali ya juu.

Naye Mjumbe kutoka Idara ya Uhandisi Misitu na Sayansi za Mazao ya Misitu, Mbonea Mweta alisema semina hizi zimekuwa sehemu ya kupata suluhisho la changamoto baada ya mafunzo na hiyo imeonekana mara baada ya kumaliza semina hiyo na kuona kuwa SUA iko vizuri kwa upande wa wanafunzi wake wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo hivyo jukumu walilonalo kwa sasa ni kujitangaza watu waone shughuli zinazofanywa na wanafunzi kutoka chuoni hapo.

# Wanafunzi wa Shule ya Sekondari wafanya ziara SUA kujifunza kilimo kwa vitendo



Wanafunzi wa kidato cha tatu wanaosoma somo la kilimo kutoka Shule ya Sekondari Wilbalda iliyopo Kabuku mkoani Tanga wametembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kupata fursa ya kuona namna kilimo kinavyofanyika kwa vitendo kupitia somo la kilimo ambalo linafundishwa shuleni kwao pamoja na kukuza ufahamu wao juu ya shughuli zinazofanywa na Chuo hicho .

Hayo yameelezwa na Venance Peter ambaye ni Mwalimu kutoka shule hiyo wakati akizungumza na SUAMEDIA kuhusiana na lengo la kutembelea SUA kwa wanafunzi wanaosoma somo hilo.

Mwl. Peter alisema kwasababu shule yao inafundisha somo la kilimo wameona ni vyema kwa wanafunzi hao kutembelea Chuo Kikuu cha SUA kwa ajili ya kujifunza kwa vitendo kwasababu SUA ina vifaa vya kisasa ambavyo kwenye taasisi zingine hawana, mfano mashine ya kukamua maziwa ya ng'ombe pamoja na kuwa na wataalam waliobobea katika kilimo.

"Tumeweza kujifunza ufugaji wa Sungura, Nguruwe, Kuku pamoja na Ng'ombe kuanzia kuzaliwa kwake mpaka ukuaji wake, vile vile tumepata nafasi ya kujifunza uzalishaji wa samaki kuanzia pale anapotaga mayai mpaka hatua ya mwisho." amesema mwl. Peter.

Aidha, Mwl. Peter amesema SUA imetoa mwanga kwa wanafunzi wao na kuwafanya warejee shuleni kwao Wilbalda tayari wakiwa wamejaa ujuzi na maarifa kuhusu somo la kilimo na anaamini wanafunzi hao watatenda kuwa mabalozi wazuri wa SUA.

Vile vile, Mwl. Peter ametoa wito kwa shule nyingine nchini ambazo zinafundisha somo la kilimo kuweza kukitumia Chuo Kikuu cha SUA katika kukuza uelewa kwa walimu wa masomo hayo pamoja na wanafunzi katika kujifunza kwa vitendo ambapo wao wameweza kunufaika kwa kwa kiasi kikubwa hali itakayowasaidia katika kukuza shughuli zao za kilimo.

Kwa upande wake, Epiphania Sembeka ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu kutoka shule hiyo amesema wamejifunza mambo mbalimbali katika ufugaji sambamba na namna ya kuweza kuikinga mifugo na magonjwa mbalimbali hivyo kupitia SUA, amepata mwangaza wa kile wanachojifunza darasani ambapo wameongeza maarifa ya kutosha hivyo ametoa rai kwa wanafunzi wenzake kutunza maarifa waliyoyapata chuoni hapo .

"Nawashukuru SUA kwa elimu ambayo ametupatia itayoweza kutusaidia kwa baadaye tuweze kuwa wakulima wakubwa na kujenga uchumi wa taifa." amesema Seberua Maganga mwanafunzi wa shule hiyo.

# Kampuni ya Uzalishaji wa Sukari Bagamoyo yaipongeza SUA kwa kutoa wahitimu bora

Uongozi wa Kampuni ya Uzalishaji wa Sukari Bagamoyo ulio chini ya Makampuni ya Bakhresa umekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kutoa wahitimu ambao wanaaminika kwa kiwango kikubwa katika mnyororo mzima wa uzalishaji wa bidhaa ya Sukari.

Akizungumza na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko SUA, Meneja Rasilimali Watu wa Kiwanda cha Sukari Bagamoyo Bw. Habibu Issah amesema kuwa kiwanda chao chenye malengo ya kuzalisha tani Laki Moja kwa mwaka kimeridhishwa sana na ushirikiano kati yao na SUA kwani umekuwa na tija kwa kuwaletea wanafunzi wanaojifunza kwa vitendo ambao wanaongeza uzalishaji.

Bw. Issah amesema ukiufuatilia mnyororo mzima wa uzalishaji wa Sukuri kuanzia shambani, umwagiliaji, uwekaji wa mbolea, uvunaji na uchakataji wa sukari yenyewe, kumekuwa na wahitimu na wanafunzi wanaofanya mazoezi kwa vitendo na wamekuwa wakifanya kazi vizuri na sio mzigo katika utendaji wao wa kazi.

Aidha, Meneja Rasilimali Watu huyo amesema kiwanda hicho ni cha kisasa na hata Teknolojia zake ni za kisasa lakini hakuna changamoto wanayopata wanapowapokea wanafunzi kutoka SUA kwani wanawapa mafunzo kidogo kama utaratibu wao na ni kwa sababu SUA imekuwa ikiwapatia nafasi ya kujifunza kwa vitendo mara kwa mara mafunzo ambayo yanawawezesha kujua teknolojia zinazoenda na wakati.

Kwa upande wake Bw. Saguti Ibrahimu ambaye ni Mtafiti Idara ya Kilimo katika Kiwanda cha Sukari Bagamoyo na pia ni mhitimu kutoa SUA amesema chuo hichi ni chuo bora kwa utoaji wa elimu kwani mafunzo waliyopata chuoni yametosha kuwafanya watimize majukumu yao pamoja na kuwepo kwa teknolojia ngeni za kisasa zaidi zinazoletwa na kiwanda.

Aidha, amewaasa vijana kujiunga na chuo hicho na waondoe fikra kuwa kilimo ni cha jembe la mkono pekee kwani sasa kuna teknolojia za kisasa nyingi ambazo kijana anaweza kufanya kilimo katika maeneo mbalimbali kama wao walivyofanikiwa kufanya kazi katika viwanda hivyo wanapaswa kuona kilimo kama fursa tofauti na zamani.

Akizungumzia lengo la kuwatembelea wanafunzi hasa katika Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko Bi. Suzana Magobeko amesema ni kujionea namna wanafunzi wahitimu na wanaofanya mafunzo kwa vitendo ili kupata taarifa zitakazosaidia kuboresha zaidi mitaala ya SUA.

Amesema pamoja na kupokea pongezi kutoka kwenye uongozi wa SUA inaona fahari kushikirikiana na Sekta binafsi kama Makampuni ya Bakhresa ambayo yamekuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa nchi kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na mazao ya kilimo lakini pia kwa kujenga uhusiano mzuri ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu, SUA kuleta wanafunzi wajifunze kwa vitendo na kiwanda kinapokuwa na nafasi za ajira basi wanafunzi wa SUA wapewe nafasi.







# SUA kushirikiana na Halmashauri ya Mpimbwe kutoa elimu na tafiti kwa wakulima na wafugaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe mkoani Katavi zimekubaliana kushirikiana kupitia vyombo vyake vya habari vya SUA Media na Mpimbwe FM katika kutoa elimu, teknolojia, ubunifu na matokeo ya utafiti katika sekta ya kilimo.

Akizungumza na ujumbe wa SUA uliofika ofisini kwake Julai 16, 2024 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe Bi. Shamim Mwariko amesema wamefurahishwa na wazo hilo la SUA kwani ili kuleta maendeleo ya kilimo nchini ni muhimu wakajua mbinu bora za kilimo.

Amesema ushirikiano kati ya SUA na Halmashauri hiyo utasaidia kufikisha elimu, teknolojia, ubunifu na matokeo ya utafiti huku akisisitiza watafiti nchini wakiwemo wa SUA kutoa matokeo ya utafiti kwa lugha rahisi ambayo inaeleweka na mkulima.

Akizungumza wakati akitoa ombi la SUA kushirikiana na Halmashauri hiyo Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko SUA Bi. Suzana Magobeko amesema Menejimenti ya SUA kupitia vikao vyake iliona ni muhimu kuunga mkono juhudi zilizofanywa na Halmashauri hiyo za kuwa na chombo cha habari Mpimbwe FM kwa kutoa maudhui yanayoweza kuwasaidia wakulima na wafugaji ili kuinua sekta hiyo nchini.

Bi. Magobeko amesema SUA itahakikisha wataalam wake katika sekta ya kilimo wanashiriki kikamilifu katika kutoa habari na maudhui kupitia Mpimbwe FM na SUA Media pia itakuwa ikipokea na kutoa habari za Halmashauri hiyo kupitia vyombo vyake vya SUA FM na mitandao yake ya kijamii.



*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe Bi. Shamim Mwariko akizungumza na ujumbe kutoka SUA (hauko pichani).*




*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko SUA Bi. Suzana Magobeko wa pili (kulia) na Msimamizi wa SUA Media Bw. Gerald Lwomile wa pili (kushoto) wakiwa na wafanyakazi wa Mpimbwe FM.*



# Watumishi epukeni mgongano wa maslahi




*Afisa Maadili Kanda ya Mashariki, Bi. Jacqueline Msumba.*

Watumishi wa umma wametakiwa kujiepusha na mngongamano wa maslahi wakati wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali ili kuwe na usawa na haki katika utoaji wa huduma kwa jamii.

Afisa Maadili Kanda ya Mashariki Bi. Jacqueline Msumba alitoa wito huo Jumatano tarehe 28.08.2024 wakati akitoa mada kuhusu mgongano wa maslahi kwa watumishi wa umma katika mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko ambapo amesema mgongano wa maslahi husababisha kupotea kwa haki wakati wa kutoa huduma.

Bi. Msumba alisema kumekuwa na watumishi wa umma ambao wamekuwa wakitumia nafasi zao kujinufaisha wenyewe badala ya kuweka mbele matarajio ya wananchi katika eneo la kazi.

Alisema ni wakati sasa wa kuendelea kujifunza namna ya kuepuka au kudhibiti mgongano wa maslahi akisema kufanya hivyo kutaongeza uwezo katika utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na kupunguza migogoro kwenye taasisi.

Bw. Nicholaus Romani mshiriki wa mafunzo hayo alisema anaamini elimu hiyo itaboresha utendaji kazi kwenye kitengo cha mawasiliano na masoko suala ambalo litapelekea ufanisi katika utendaji kazi pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko yaliyofadhiliwa na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi yanalenga kuboresha na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.








*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima akiongea na Wanajumuiya wa SUA na waalikwa wengine (hawapo pichani) waliojitokeza katika siku ya kufunga Maadhimisho ya Miaka 50 ya kuanzishwa kwa Kitivo cha Mafunzo ya Misitu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

# RC Malima awataka wataalamu wa misitu SUA kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima amewataka Wataalamu wa Misitu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuhimiza utekelezaji wa utunzaji na uendelezaji wa misitu nchini kwa manufaa ya vizazi vya sasa na baadaye.

Alibainisha hayo katika siku ya kufunga Maadhimisho ya jubilei ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Kitivo cha Mafunzo ya Misitu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, ambapo amesema kitu wanachotakiwa kukifanya ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuisadia kupata uelewa wa umuhimu wa uhifadhi wa misitu katika maeneo yote kwa ajili ya kukiwezesha kizazi kijacho kuja kunufaika na misitu na mazingira kiujumla.

Aidha, Malima alisema wataalamu kutoka SUA wanapaswa kuifahamisha jamii athari zinazotokea kutokana na uharibifu wa misitu ambao kwa kiasi kikubwa unasababishwa na shughuli za binadamu ikiwemo kuchoma mkaa, kukata kuni na shughuli za kilimo hasa maeneo ya pembezoni mwa miji.

Kwa upande wake mtaalamu wa sheria za misitu kutoka SUA, Dr. Mectrida Kaijage alisema wataalamu wana wajibu wa kutunga miswada na kupeleka kwa serikali ili kuhamasisha matumizi sahihi ya rasilimali za misitu lakini pia amezitaka taasisi kama SUA kutafuta washirika ambao watashirikiana nao katika uratibu wa uhifadhi misitu.

"Natumaini wataalamu kutoka SUA mtaendelea kufanya tafiti zenye tija kuhusiana na misitu ikiwemo njia sahihi za kutatua changamoto za kidunia ambazo zinaathiri misitu na mazao yake pamoja na tafiti za kisayansi za misitu", alisema Bi. Metrida Kaijage.

Naye Prof. August Temu ambaye pia ni mtaalamu wa misitu kutoka SUA alisema anaiona Tanzania ikiendelea kufanya vizuri katika utunzaji wa misitu kwani SUA inaendelea kuzalisha Wataalam wengi wa Misitu ambao watazidi kuwa vinara wa utunzaji misitu na rasilimali zake kwa manufaa makubwa ya jamii na kizazi kijacho.

"Miaka 50 ijayo naiona Tanzania ikifikia hatua ya nchi kama Finland na China ambazo zinatumia vizuri mazao ya misitu kwani katika nchi hizo kila zao la msitu lina matumizi katika viwanda vya uzalishaji ma-

lighafi, ambazo zinatumika kuinua uchumi wa nchi hivvo naamini Tanzania itafikia hatua hiyo kama tu watu wataweza kutunza misitu kikamilifu", alisema Prof. Temu

Mhe. Diwani wa Kata ya Magadu Bw. Juma Issa Kiduka amesema, elimu inayotolewa na SUA imepunguza matukio ambayo yalikua yanahatarisha utunzaji wa misitu ikiwemo uchomaji moto katika maeneo ya milima ambayo imezungukwa na misitu, Hivyo amewaomba wataalamu kutoka Chuo hicho kuendelea kutoa elimu na kuwafikia wananchi wengi zaidi hasa wa kata ya Magadu ili kuendelea kupunguza athari ambazo zinaweza kusababishwa na shughuli za binadamu kwenye misitu.











# SUA yanunua Mtambo wa kuchimba visima




*Mtambo wa kuchimba visima.*

Katika kukabiliana na uhaba wa maji, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimenunua Mtambo wa kuchimba visima ambao umeelezwa kuwa mbali na kutatua changamoto ya maji pia utasaidia katika kufundishia kwa vitendo wanafunzi wanaosoma Shahada zinazoendana na Uhandisi wa Maji ikiwa ni sehemu ya ufadhili wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi.

Akizungumza wakati wa kuupokea Mtambo huo, tukio lililofanyika Kampasi ya Edward Moringe, siku ya Jumatano, Septemba 11, 2024, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji SUA, Prof. Ibrahimu Mjemah alisema, SUA iliweka dhamira ya kununua mtambo mkubwa wa kuchimba visima ili usaidie kupunguza uhaba wa maji.

Upatikanaji wa maji yakutosha utasaidia katika kilimo cha umwagiliaji hasa katika Mashamba ya Mfano ya Chuo. Vilevile, Mtambo huo utasaidia kuboresha ufundishaji kwa vitendo wanafunzi na wadau wengine jinsi ya uchimbaji wa visima na kuhusu namna bora ya kufanya uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji.

"Mtambo huu utasaidia kuongeza upatikanaji wa maji hapa chuoni lakini pia utasaidia kufundishia wanafunzi wanasoma shahada zinazohusika na Uhandisi wa Kilimo katika uchimbaji wa visima na umwagiliaji jambo ambalo sisi tunaliona litakuwa na tija kwa wakati huu na wakati ujao kwani tutaweza kuandaa wataalamu wa baadaye", alisema, Prof. Mjemah.

Alisema pamoja na mtambo huo wenye uwezo wa kuchimba kisima chenye urefu wa mita zaidi ya 500 kwenda chini ambao utawezesha Chuo kukabiliana na uhaba wa maji katika Kampasi zake zote pia utaweza kutoa huduma kwa wananchi wa mikoa jirani ambao watahitaji huduma ya maji katika maeneo ambayo yana uhaba wa maji kwa matumizi ya nyumbani ama shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

Katika hatua nyingine, Prof. Mjemah aliushukuru Mradi wa HEET kwa kuwezesha ununuzi wa Mtambo huo mkubwa wa kuchimba visima, akisema kwa kufanya hivyo kutaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu hasa ya kilimo kwa upatikanaji wa maji ya uhakika kwenye Mashamba ya Mfano ya Chuo.



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa akiwa ndani ya Mtambo wa kuchimba visima ulionunuliwa na SUA kupitia mMadi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).*



**Jarida limetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania
**Simu:** 255-023-2640006/7/8/9,
**Baruapepe:** communicationandmarketing@sua.ac.tz